## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

1. Social Action Trust Fund (SATF) ni taasisi iliyoanzishwa mwaka 1998, kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali katika kutoa huduma kwa Watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kupunguza athari zitokanazo na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sasa SATF inafanya kazi katika mikoa 17 na Halmashauri 37 za Tanzania. Huduma zinazotolewa ni pamoja Elimu, Afya, Ulinzi wa Mtoto pamoja na afua za kuimarisha uchumi katika ngazi ya kaya.
2. SATF kwa kushirikiana na Chuo Cha VETA Kongwa - imeandaa mafunzo ya muda wa miezi mitatu (3) yatakayofanyika katika Chuo Cha VETA Kongwa kilichopo Wilaya ya Kongwa,Mkoani Dodoma . Fani zitakazotolewa katika mafunzo hayo ni pamoja na;- ***Ufundi wa Magari, Ufundi Umeme, Ujenzi, Ushonaji, Mapambo, Upishi, na Ususi.***

3. SATF inapenda kuwatangazia Vijana wa kitanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25 katika Wilaya zifuatazo; Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa,Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma na Wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara kutuma maombi ya kujiunga na mafunzo haya.
   SATF itagharamia gharama zote za mafunzo haya ikiwa ni pamoja na ada, malazi pamoja na chakula kwa muda wote wa mafunzo.
4. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi inayopatikana katika ofisi za shirika la FPCT-Chamwino ama katika ofisi ya Afisa Maendeleo wa Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa,Wilaya ya Chamwino;na kwa waombaji watokao Mkoa wa Manyara kwenye Ofisi za Shirika la V4Y ama katika ofisi ya Afisa Maendeleo Wilaya ya Simanjiro ama katika tovuti www.satf.or.tz. Fomu iliyojazwa irudishwe katika ofisi mojawapo kati ya Ofisi ya Afisa Maendelo wilaya unayotoka au ofisi za FPCT Chamwino- zilizopo Dodoma Mjini kwa wale wa Wilaya za Kongwa na Chamwino au ofisi za V4Y zilizopo Arusha Mjini kwa wale wa Wilaya ya Simanjiro, kabla ya tarehe 16 Septemba,2026

5. Fomu za maombi ziambatane na nyaraka zifuatazo;
   i. Kitambulisho cha uraia au kadi ya mpiga kura,
   ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa au kiapo cha ushahidi wa kuzaliwa,
   iii. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji; na
   iv. Picha mbili za paspoti *(ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma)*
6. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:
   i. Awe Mtanzania mwenye umri wa miaka isiyopungua 18 na isiyozidi 25
   ii. Awe kijana nje ya shule aliyemaliza Elimu ya msingi au sekondari
   iii. Awe na nia ya dhati ya kujifunza ujuzi aliouchagua.
   iv. Awe tayari kujiunga kati ya kozi mojawapo tajwa.
   v. Vijana wenye ulemavu na wanaotoka kwenye kaya zilizo chini ya mpango wa TASAF na SATF wanasisitizwa kuomba fursa hii na watapewa kipaumbele katika mafunzo haya.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi SATF**
**3 Septemba, 2026**

*NB:*

- ***Watakaokidhi vigezo na masharti tu ndio watakaochaguliwa***.
- ***Maelekezo zaidi na taratibu zote za kujiunga yanapatikana pia kwenye ofisi za FPCT Chamwino - Dodoma Mjini - Bi. Alice Madelele 0744 952 577 au ofisi za V4Y-Arusha Mjini Bw.David Munene 0754 306 250 - au Bi Joselina Mutoka 0768 026 544.***